

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA
Barua zote ziandikwe kwa: Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,



Simu Na 023 2402738,
Fax Na 023 402706
Unapojibu tafadhali taja:

S.L.P. 10,
MKURANGA,
PWANI.

Kumb. Na. MDC/L.20/6/VOL.LXX/97 10/3/2021

Mkurugenzi Mkuu,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P.938,

Dar es salaam

YAH: KUITAMBULISHA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA TENG DA FOOTWEAR LIMITED KUNUNUA NA KUPIMISHA KIWANJA NA.37 KITALU'F'MWANAMBAYA, WILAYA YA MKURANGA

Rejea mada tajwa hapo juu.


Ninakujulisha kwamba, kiwanja tajwa hapo juu kimetokana na upimaji wa eneo lililonunuliwa na kampuni na kisha kupimwa kwa kuzingatia Ramani ya Mipango Miji Na.19/MKR/05/022011 matumizi ya Ghala

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999, fungu la 19-20 na Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na.26 ya mwaka 1997, aidha kwa kuzingatia fungu la 12 na 179 Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 na Tangazo la Serikali Na.72 la tarehe 4/5/2001, kanuni za Ardhi za 2001, kanuni ya 9C(v), kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

Halmashauri ya Wilaya inaitambulisha Kampuni hii kutoka nje ya nchi kwako ili iweze kupatiwa Certificate of Incentive yenye kuonyesha namba ya kiwanja uwekezaji utakapofanyika ili kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya kuandaa **Designation for Investment-Land form Na.1** ili viwanja hiki kitangazwe kuwa cha Uwekezaji na hatimaye kuingizwa katika **kamati ya Ugawaji wa Ardhi Taifa.**

Nawasilisha kwako kwa hatua zaidi, nimeambatanisha nyaraka muhimu kwa urahisi wa rejea (**Hati ya ununuzi wa eneo, Usajili wa Kampuni, Ramani ya Mipango Miji na Upimaji**).

Kwa hatua zako muhimu.


Chagiye R.M
Kny.Mkurugenzi Mtendaji (W),
Mkuranga.

Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W)
Mkuranga -Kwa taarifa

Teng Da Footwear Limited
Dar es salaam -Fuatilia nyaraka husika TIC